

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI CHOMA,

S.L.P 222,

IGUNGA.

10/12/2020.

**Kumb. Na. CHSS/J1/Vol. 01/13/2020/2021**

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

JINA LA MZAZI WA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

KIJIJI ANACHOTOKA \_\_\_\_\_

SHULE ALIYOSOMA \_\_\_\_\_

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHOMA**

### **KWA MWAKA WA MASOMO 2021**

#### **1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha \_\_\_\_\_ katika shule hii mwaka \_\_\_\_\_ shule ya sekondari Choma ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko. Shule hii ipo katika KATA ya Choma, Tarafa ya Manonga wilaya ya Igunga.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shulenii siku hiyo bila kukosa, ukichelewa Zaidi ya siku saba (7) yaani baada ya tarehe 18/01/2021 utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kukamatwa na Mgambo na kupelekwa kwa mtendaji wa kata na hata kufikishwa Mahakamani.

#### **2. MAMBO MUHIMU YAKUZINGATIA**

##### **(i) SARE ZA SHULE YA SEKONDARI CHOMA**

###### **(A) WASICHANA**

- (I) SKETI yenyeye rangi ya **BLUU ILIYOKOLEA** ya kawaida yaani yenyeye marinda na isiwe **FUPI** \* Urefu wa sketi kutoka magotini uwe nchi 6 kwenda chini.
- (II) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- (III) Viatu vya Ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi.
- (IV) Soksi nyeupe na ndefu zinazofika magotini jozi mbili.
- (V) **T-SHIRT** moja au mbili rangi ya bluu zenye kola pamoja na Nembo ya shule.
- (VI) **SWETA** ya Rangi ya kijivu.

**NB:** kwa wasichana wa Kiislamu watakaopenda kushona au kuvaan **HIJABU** rangi zifanane na sare ya shule.

###### **(B) WAVULANA**

- (I) Suruali nzito (Estem 1) rangi ya Bluu iliyokolea yenyeye marinda, **HAKIKISHA** isiwe **MODO** (yaani inayobana).  
**NB:** Suruali ya kubana na ya kihuni haitakubalika.
- (II) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- (III) Viatu vya Ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi.
- (IV) Soksi nyeusi na ndefu jozi mbili.
- (V) **T-SHIRT** moja au mbili rangi ya **BLUU** zenye kola pamoja na

Nembo ya shule.

(VI) SWETA rangi ya kijivu.

**(ii) MAVAZI YA MICHEZO**

(I) T-SHIRT na TRUCK SUIT zote rangi ya BLUU

(II) Raba pamoja na Bukta.

**NB:** Mavazi ya michezo yanayobana mwili **HAYATARUHUSIWA**.

**(iii) VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

(I) Madaftari makubwa ( 3 au 4 quire) yawe TISA (9)

(II) Kalamu

(III) Penseli

(IV) Rula

(V) Mathematical seti ( mkebe wa Hesabu )

**NB:** Mwanafunzi anaporipoti shulen i alete faili kwaajili ya kutunzia kumbukumbu zake, ikiwa ni pamoja na matokeo yake ya mitihani.

**(iv) KWA WANAFUNZI WA KIKE WATAKAOKAA HOSTELI**

Shule ya sekondari Choma ina **HOSTELI NZURI TENA YENYE UMEME WA GRID YA TAIFA** kwaajili ya wanafunzi wa **KIKE (WASICHANA)**, Hivyo basi wasichana wote wanalazimika kukaa Hosteli ili waweze kuwa na muda wa kutosha wa kusoma.

**(I) MAHITAJI YA HOSTELI**

- ❖ Shuka mbili (2) za Bluu bahari, shuka mbili (2) za pinki na nguo za Ndani za kutosha.
- ❖ Ndoo mbili (2) za lita kumi, beseni moja, galoni moja ya lita 5, dawa ya meno.
- ❖ Taulo moja, chandarua, godoro dogo ya nchi mbili na nusu.
- ❖ Fagio moja la kawaida, fagio la kukaushia maji (drier), vifaa vya kufanyia usafi.
- ❖ Sahani, kikombe cha plastiki, kijiko, sanduku imara la kuhifadhi vitu vyake na kufuli.

Ili kuondoa usumbufu kwa wazazi wa kununua nguo nyingi mwanafunzi wa Hostel atakapomaliza muda wa vipindi na atakapokuwa anajisomea wakati wa usiku atatakiwa kuva **SKETI** ya Rangi ya Damu ya mzee na T-shirt ya shule tu! na si nguo nyingine yoyote (akionekana amevaa vazi lingine atakuwa amefanya kosa)

Mwanafunzi wa Hostel atakapokuwa anakwenda Kanisani au Msikitini atatakiwa kuva mavazi ya shule tu! Na si vinginevyo.

**(II) KWA UPANDE WA HUDUMA YA CHAKULA**

**NB:** IELEWEKE WAZI HUDUMA YA CHAKULA KWA MWANAFUNZI ATAKAYEKAA HOSTELI ITATOLEWA NA MZAZI WA MWANAFUNZI KATIKA KIPINDI CHOTE CHA MASOMO NA USIMAMIZI WAKE UPO CHINI YA KAMATI YA WAZAZI.

- (a) MAHITAJI YA CHAKULA KWA MWANAFUNZI ANAYEKAA HOSTELI KWA ROBO MUHULA (MIEZI 3) NI KAMA IFUATAVYO; -**
- ❖ **MAHINDI DEBE MBILI (2), MAHARAGE KILO 15, MAFUTA YA KUPIKIA LITA MBILI (2)**

❖ **PESA TASLIM TSH 18,000/=** ( Hii ni kwaajili ya mahitaji mengine kama kununua chumvi ikiwa ni pamoja na kumlipa mpishi)

**(b) MAHITAJI YA CHAKULA KWA MWANAFUNZI WA KUTWA YAANI ASIYEKAA HOSTELI (KWAAJILI YA CHAKULA CHA MCHANNA TU!) KWA ROBO MUHULA:**

**Mchele kilo 15, Maharage kilo 5, Mafuta ya kupikia lita 1 na Fedha Taslim Tsh. 4,000/=** (Pesa hii ni kwaajili ya kununulia mahitaji mengine kama Chumvi, Vitunguu, Nyanya, kuni ikiwa ni pamoja na kumlipa Mpishi)

**NB:** Mzazi unahimizwa kuchangia michango hiyo ili mtoto wako aweze kusoma vizuri bila kusumbuliwa na Njaa.

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII NI;-**

Shule inaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenyе dhamana ya Elimu nchini pamoja na Ofisi ya Raisi TAMISEMI yenyе jukumu la Usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi au walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la Lazima.
- ii. Mahudhurio mazuri darasani wakati wote wa vipindi, pamoja na mahudhurio mazuri katika shughuli mbalimbali za ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni Lazima.
- iii. Kushiriki kwa makini kufanya au kutekeleza shughuli zote wakati wa jioni baada ya vipindi au masomo.
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- v. Kutii na kuheshimu Wimbo wa Taifana Bendera ya Taifa.
- vi. Kuvalaa Sare ya Shule wakati wote unapokuwa kwenye mazingira ya shule na unapokuwa kwenye safari za kishule au popote pale utakapotakiwa kufanya hivyo.
- vii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- viii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa kama mwanafunzi wa shule hii na hata utakapohitimu masomo yako.
- ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.
- x. Ni makosa kisheria kuhudhuria au kuonekana katika kumbi za starehe iwe ni kwenye sherehe au vinginevyo.

**SEHEMU IFUATAYO IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE MBELE YA MZAZI AU MLEZI WAKE**

Mimi \_\_\_\_\_ ninatokea  
kijiji cha \_\_\_\_\_ nimezaliwa tarehe \_\_\_\_\_ ambaye ni  
mwanafunzi wa shule hii nimesoma na kuelewa masharti yote, sharia pamoja na kanuni za shule  
nakubali kuziflata kikamilifu na sitashiriki katika **MGOMO, FUJO** na Makosa mengine  
yoyote ya jinai.

Saini ya Mwanafunzi:

---

**SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi

---

ambaye ni mzazi au mlezi wa

---

nakiri nimesoma maelekezo yote yaliyobainishwa katika FOMU hii kikamilifu na kuelewa vizuri, hivyo basi nakubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule hii ya sekondari Choma.

Saini ya mzazi au mlezi wa Mwanafunzi:

---

Imetolewa na uongozi wa Shule ya sekondari Choma,

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHOMA!**

---

**WILLIAM EMIDI AUGUSTINE  
MKUU WA SHULE**